OFISI YA RAIS-TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI KIYOWELA S.L.P 31 MGOLOLO.

TAREHE **12.12.2020.**

KUMB.NA.ED/KYSS/JI. /VOL 01. /21

JINA LA MWANAFUNZI

……..

……

……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIYOWELA WILAYA YA MUFINDI MKOA WA IRINGA MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI.

- Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika shule hii mwaka **2021.**
- Ni matumaini yangu kuwa utaikubali nafasi hii uliyopewa na kushirikiana na wanafunzi wenzako,walimu na wafanyakazi wote katika kutekeleza malengo ya elimu.
- Kumbuka kuwa **NIDHAMU** ndiyo msingi wa mafanikio ya elimu.
- Shule hii ipo umbali wa kilomita 115 kutoka mji wa Mafinga na ipo katika kijiji cha Isaula ,kata ya Kiyowela,tarafa ya Kasanga,wilaya ya Mufindi,mkoa wa Iringa.
- Shule hii ni ya kutwa na ni mchanganyiko (wavulana na wasichana).

2.0 KUFUNGUA SHULE.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **11.01.2021.** Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11.01.2021** ukiwa na mahitaji ya shule kama ilivyoagizwa.

3.0 MASOMO YANAYOFUNDISHWA.

Masomo yanayofundishwa katika shule hii ni Hisabati, Jiografia, Kiswahili,Uraia,Historia,Kiingereza,Fizikia,Biolojia,Kemia na literature kwa kidato cha tatu nan ne.

4.0 VIFAA VYA TAALUMA.

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo;

- Daftari 10 na kuendelea(counter books) na daftari ndogo 10
- Mkebe wa hisabati(mathematical set)
- Kalamu za wino (pen) bluu au nyeusi
- Kalamu za mkaa(pencel)
- Rula
- Mfuko wa kubebea daftari(begi)
- Dictionary 01 (kamusi ya kiingereza kwa kiingereza).
- Faili kubwa (flat file) kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mitihani.

5.0 SARE ZA SHULE.

5.1 SARE YA WAVULANA

- Suruali mbili (02) kitambaa cha rangi ya" jani la mgomba namba moja" zilizoshonwa kwa heshima na zisizobana.
- Tai moja rangi ya jani la mgomba (Ni sehemu ya sare ya shule)
- Shati mbili (2) nyeupe zenye mikono mifupi (tetron).
- Viatu vya ngozi jozi mbili vyeusi vya kufunga na kamba. Visiwe buti za kijeshi na visivyo na kisigino kirefu.
- Soksi nyeusi jozi mbili(2)
- Sweta moja (1) yenye rangi ya jani la mgomba na yenye shingo ya V.

5.2 WASICHANA

- Sketi mbili (2). Moja kitambaa cha rangi ya" jani la mgomba namba moja" mshono wa sketizote mbili ni **LINDA BOX MBELE NA NYUMA NA PEMBENI MALINDA YA KAWAIDA PANDE ZOTE** zenye urefu wa nchi nne toka magotini. **SKETI FUPI** na zenye kubana hazitakubalika kuvaliwa shuleni.

- Tai moja rangi ya “jani la mgomba” (Ni sehemu ya sare ya shule)
- Shati mbili (2) nyeupe za mikono mifupi(tetron).
- Viatu vya ngozi jozi mbilii vyeusi vya kufunga na kamba.Viwe vya kufunika na Visiwe na kisigino kirefu.
- Soksi nyeupe jozi mbili (2).
- Rangi ya hijabu ni nyeupe.
- Sweta moja (1) yenye rangi ya jani la mgomba yenye shingo ya v.

6.0SARE YA MICHEZO

- Tracksuits za rangi ya blue(jozi moja au zaidi)
- Tshirt ya njano
- Raba/viatu vya michezo

7.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu,Sayansi,Teknolojia na Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumula usimamizi na uendeshaji wa elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo katika kipindi chote cha uanafunzi wako:

- Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- Kutunza mali za umma.

7.1 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- Wizi
- Uasherati na ushoga
- ubakaji
- Ulevi wa pombe,uvutaji bangi na madawa ya kulevya
- Kupiga au kupigana
- Makosa ya jinai
- Kudharau/kuharibu bendera ya taifa
- Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
- Kutoa mimba
- Kukataa adhabu kwa makusudi
- Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- Kuwa na simu ya mkononi
- Kuoa au kuolewa
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

8.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI MWANAFUNZI ANAPORIPOTI.

- Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali.

KARIBU SANA KIYOWELA SEKONDARI.

……

MWL.HENRY S. LUPONDO

MKUU WA SHULE

0752151697.

PRESI DENT' S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATIONANDLOCALGOVERNMENT MUFINDI DISRICT COUNCIL KIYOWELA SECONDARY SCHOOL MEDICAL EXAMINATIONFORM tobe completedby medical officers ina recognized Hospital in respectofall new entrants of Kiyowela SecondarySchool

Full Name…….

Age…….

1.Blood comment (red&whit e) …….

3.Urine examination…….

4.Stool examination……

5.Syphilistest ……

6.T.B.test …….

7.Ear test ……

8.Spleen…….

9.Abdominal …….

10.Eye test …….

11.Additional informationorany other physical, hereditaryor infectious diseases

……

……

……

……

Treatment after examination

……

……

……

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the above mentionedhasbeen examinedand found fit to pursue for further education

Signature……

Designation……

Station……

Official stamp……

Date……

N.BFomu hii ijazwenaMganga katika Hospitali inayotambulikana serikali.